**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 16 Juni, 2021**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Milioni Mia Tisa Themanini na Tisa, Laki Saba na Elfu Themanini na Nne Kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia siku ya Tarehe Thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Mbili na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

136. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuna ongezeko kubwa la idadi ya watoto waliofikia umri wa kuanza elimu ya maandalizi Zanzibar.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani katika kukabiliana na upungufu wa madarasa ya maandalizi.

(b) Je, ni kwa kiasi gani Serikali inajiandaa kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu wa maandalizi.

139. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Skuli za Msingi pamoja na Maandalizi sasa ziko chini ya uongozi na majengo ya pamoja hali inayopelekea watoto wadogo kuchanganyika na wakubwa.

(a) Je, Serikali inaonaje kama skuli za maandalizi zingetenganishwa na skuli za msingi ili kuwalinda watoto wadogo wa maandalizi dhidi ya vitendo vya udhalilishaji.

(b) Je, Wizara inajipangaje kuyaimarisha mazingira ya skuli za msingi ili yawe rafiki kwa wanafunzi wa Maandalizi.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

53. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Wananchi wa kijiji cha Kiuyu Mbuyuni wamekuwa wakitoa taarifa kwa muda mrefu juu ya uwepo wa mrundikano wa madawa yaliyopitwa na wakati (expired date) katika Kituo cha Afya kilichopo kijijini hapo ambapo wagonjwa pamoja na wafanyakazi wamekuwa na hofu ya kuhatarisha afya zao.

(a) Je, ni taasisi au kitengo gani kilichopewa dhamana kwa mujibu wa sheria katika kuangamiza madawa hayo.

(b) Ni lini taasisi au kitengo hicho kitafanyakazi kwa wakati ili kuepusha madhara yanayoweza kuepukika.

215. MHESHIMIWA PROF.OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imefanikiwa kufunga mfumo mzuri wa mawasiliano wa TEHAMA katika Hospital Kuu ya Rufaa ili kuweza kurahisisha huduma za kimatibabu kutoka kada moja ya afya kwenda nyengine. Licha ya jitihada hizo nzuri za Serikali mfumo huo umekuwa ukileta mwanya wa upotevu wa madawa kama watakuwepo watendaji wasio waaminifu.

(a) Je, kwa kiasi gani mfumo huo unazuia mianya ya undanganyifu juu ya uwepo au kutokuwepo kwa dawa kama mgonjwa alivyoelezwa na daktari.

(b) Je, Wizara ina ratiba gani ya Ukaguzi wa mifumo yake ya TEHAMA ili kuiboresha kuendana na wakati na usalama stahiki kwa wakati husika.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

94. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, kuna utaratibu gani wa Maafisa wa Elimu wa ngazi ya Wilaya na Mkoa, kupewa mafuta ili waende kwenye maeneo yao ya kazi.

137. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Masuala ya udhalilishaji yanaongezeka sana katika jamii kwa kadri siku zinavyoendelea. Kwa kuwa watoto ndio waathirika wakuu wa udhalilishaji huo.

(a) Je, Serikali haioni kuna haja ya kuanzisha somo la elimu ya kujikinga na udhalilishaji katika ngazi ya elimu za maandalizi na msingi.

(b) Je, walimu wanapatiwa elimu juu ya namna ya kuwasaidia watoto waliodhalilishwa.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

73. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kabla ya ujenzi wa barabara ya Bububu hadi Kwanyanya Serikali iliweka taa za barabarani katika eneo hilo. Hata hivyo, taa hizo ziling’olewa wakati wa ujenzi wa barabara hiyo na hivi sasa tayari ujenzi wa barabra hiyo umekamilika.

Je, ni lini Serikali itazirejesha tena taa hizo ili kuleta usalama kwa watumiaji wa barabara hiyo wakati wa usiku.

164. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa, barabara ya Wawi Uwandani kupitia Vikunguni ni ya muda mrefu na ina umuhimu mkubwa kwa wananchi. Na kwa kuwa barabara hiyo kwa sasa ni mbovu na haipitiki hata kwa gari za abiria na kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wanaoitumia barabara hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami, ili iweze kupitika muda wote.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane Ishirini na Tisa, Milioni Mia Tisa Themanini na Tisa Laki Saba na Elfu Themanini na Nne Kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia siku ya Tarehe Thelathini Juni, Mwaka wa Elfu Mbili na Ishirini na Mbili na Kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo Pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kurekebisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa Mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**16 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**